



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA



HALMASHAURI YA WILAYA YA BIHARAMULO

Unapojibu Tafadhali Taja:

Kumb Na.BDC/4/32/VOL.II/30

30/09/2021

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo amepokea kibali cha Ajira Mbadala kutoka kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Kwa hiyo, anawatangazia Watanzania wote wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi 03 kama inavyoonekana hapa chini:-

1. MSAIDIZI WA KUMBUKUMBU DARAJA LA II-(NAFASI 02) TGS B.

SIFA ZA MWOMBAJI.

- Awe na elimu ya kidato cha IV au cha VI.
- Awe na cheti cha Astashahada (Technician Certificate- NTA LEVEL 5) cha Utunzaji wa Kumbukumbu katika moja wapo ya fani za Afya, Masjala, Mahakama na Ardhi.

MAJUKUMU YA KAZI.

- Kutafuta Kumbukumbu/ Nyaraka/Mafaili yanayohitajika na wasomaji.
- Kuthibiti upokeaji, uandikishaji wa Kumbukumbu / Nyaraka.
- Kuchambua, Kuorodhesha na kupanga kumbukumbu/ Nyaraka katika makundi kulingana na somo husika (Classification and Boxing) kwa ajili ya matumizi ya ofisi.
- Kuweka / kupanga kumbukumbu, nyaraka katika reki(file racks/cabinets) katika masjala / vyumba vya kuhifadhia kumbukumbu.
- Kuweka Kumbukumbu (barua, nyaraka nk) katika mafaili.
- Kushughulikia maombi ya kumbukumbu/ nyaraka kutoka Taasisi za Serikali.

2. DEREVA DARAJA LA II – (NAFASI 01) TGS B.

SIFA ZA MWOMBAJI:-

- Kuajiriwa mwenye cheti cha Kidato cha Nne (Form IV) na leseni ya Daraja la E au C1 ya uendeshaji magari ambayo amefanyia kazi kwa muda usiopungua mwaka mmoja bila kusababisha ajali.

